

# Mradi wa Uimarishaji wa Huduma Muhimu za Afya (MUHUMA)

*(Mradi wa pamoja kati ya Wizara ya Afya na Shirika la Kimataifa la Maendeleo na Utafiti la Canada (IDRC)*

## Muhtasari Na. 3: Bajeti ya Huduma za Afya




*Chombo hiki kinatumika katika hatua tatu za uandaaji wa mipango.*




# Picha ni bora kuliko maneno

Mradi wa Uimarishaji wa Huduma Muhimu za Afya (MUHUMA), ni mradi wa pamoja kati ya Wizara ya Afya na Shirika la Kimataifa la Maendeleo na Utafiti la Canada (IDRC). Mradi huu umekuwa ukifanya juhudi za kutekeleza utoaji wa huduma bora na kutafiti mbinu endelevu za kuboresha mfumo mzima wa utoaji huduma ya afya katika ngazi ya wilaya. Muhtasari wa habari za MUHUMA una lengo la kuwafahamisha wananchi matokeo ya tafiti zake na mafunzo ambayo imeyapata. Hii ikiwa ni pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa tafiti zake ambazo zimeonyesha mafanikio makubwa katika nyanja za huduma ya afya.

**Maelezo ya awali: Uimarishaji wa Menejimenti ya Afya katika ngazi ya Halmashauri ya Wilaya**

Hapa Tanzania, Mipango inayoambatana na Bajeti kwenye Sekta ya afya kwenye ngazi ya wilaya ni zoezi gumu na wakati mwingine mipango hiyo huwa katika kurasa zaidi ya 40. Jumla ya fedha katika mipango inaweza kuwa katika kiwango cha mamilioni ya fedha katika bajeti ambayo inahusu zaidi ya vifungu vya kasma 1,000. Matokeo ya mwisho - Mpango wa Afya katika ngazi ya wilaya unakuwa ni mgumu kuuelewa na mara nyingi Timu ya Menejimenti ya Afya katika Halmashauri ya Wilaya pamoja na wahisani wanapata taabu katika kujua hali halisi ya jinsi fedha za bajeti zitakavyotumika.

Kwa kurejea mpango wake, Timu ya Menejimenti ya Afya katika Halmamshauri ya Wilaya ni lazima iwe tayari kuona jinsi rasilimali kidogo iliyopo inavyoweza kutumika kwa kuzingatia kipaumbele katika mipango waliojiwekea. Ni jambo muhimu vile vile kwamba Timu ya Menejimenti ya Afya katika Halmashauri ya Wilaya iwe katika hali ya kuweza kupima utekelezaji wa mipango yake ili mwishoni mwa kila mwaka ijue matumizi halisi ya fedha kwa kulingana na umuhimu wa mipango waliyojipangia.

**Tatizo ambalo linashughulikiwa**

"Habari ambazo zimejaa wingi wa takwimu" zinaifanya bajeti iwe vigumu kueleweka na kuifanyia uchambuzi kwa ajili ya uandaaji wa mipango na utekelezaji wake."

**Suluhisho**

Bajeti ya huduma za Afya imetengenezwa ili kuisaidia timu ya Menejimenti ya Afya katika Halmashauri ya Wilaya iweze kufanya

tathmini ya bajeti yake na matumizi kwa kutoa muhtasari wa ukurasa mmoja na "michoro"mbalimbali ambayo inatoa picha ya mpango wa mwaka mzima. Bajeti hii inaweza kuunganishwa katika Jedwali linaloonyesha magonjwa yanayojitokeza zaidi katika wilaya (Angalia Muhtasari Na: 1) ili bajeti ziweze kutengenezwa sambamba na mahitaji muhimu kama ilivyooanishwa kwenye jedwali hili.
Zana hii imeundwa kwenye programu ya MS Excel na kuhifadhiwa kwenye disketi. Inahitaji ujuzi kidogo sana wa kompyuta ili iweze kutumika.
Kwa utaratibu huu wa kuifanya bajeti iwe rahisi kusomeka na kueleweka, Bajeti ya Huduma za Afya inatekeleza mahitaji yafuatavyo:

- Inatoa tathmini sahihi ya bajeti pamoja na matumizi kwa kulinganisha na umuhimu wa mipango.
- Inaonesha uwezo wa fedha zilizopo kama ilivyopitishwa na Timu ya Menejimenti ya Afya katika Halmashauri ya wilaya na jinsi rasilimali hiyo ilivyogawanywa.
- Inazingatia michango ya vyanzo vyote vya mapato, kutoka Serikalini, asasi zisizo za Kiserikali, Jamii na Sekta binafsi.
- Inaonyesha mipangilio ya fedha katika maeneo muhimu ya huduma ya afya na utekelezaji wa mipango.
- Inalinganisha kasma mbalimbali kwenye bajeti na matumzi halisi.
- Inajiridhisha kwa uwajibikaji na uwazi.

Zana hii inaonyesha makadirio muhimu, kama vile jinsi ya kuchangia huduma ya kinga na tiba au mtaji uliopo kwa kulinganisha na matumzi. Mwishoni inatoa michoro ambayo inakuwa rahisi kuichambua bajeti kwa kulinganisha na miongozo mbalimbali kutoka Wizara ya Afya.

## Matumizi ya zana hii

Kila mwaka, wilaya hupatiwa zana hii. Zana hii huwa imejaa taarifa nyingi kama vile idadi ya watu katika wilaya, gharama na bei za madawa, ubadilishaji wa fedha kwa viwango vya fedha za kimataifa, masurufu na miongozo ya Wizara ya Afya.
Mfumo huu unatumika katika hatua tatu ya uandaaji wa mipango. Kabla ya kuanza kwa mwaka wa fedha, Timu ya Menejimenti ya Afya katika Halmashauri ya Wilaya kwanza hutoa muhtasari wa awali wa mpango. Katika hatua ya kwanza, wajumbe wanatumia Jedwali linaloonyesha kiwango cha magonjwa ili liweze kuwasaidia wajumbe katika kupanga matumizi ya fedha kutokana na umuhimu unaojitokeza.
Kwa msaada wa Bajeti ya Huduma za Afya za Wilaya, wajumbe wanaweza kupanga mipango yao kwa kulingana na kipaumbele watakachokuwa wamejiwekea. Hatua ya mwisho ya mpango inatengenezwa mwanzoni mwa mwaka wa fedha wakati ambapo mgawanyo wa fedha katika bajeti unapokuwa umekwisha kuidhinishwa.
Mwishoni mwa mwaka, chombo hicho hicho inatumika kulinganisha bajeti na matumizi halisi ya fedha zilizoidhinishwa.
Zaidi ya hapo hii ni mojawapo ya njia za kuzisaidia Timu za Menejimenti za Afya katika Halmashauri za Wilaya ili ziweze kuchukua hatua madhubuti zaidi katika uandaaji wa mipango ya maendeleo.
Bajeti ya Huduma za Afya za Wilaya inaweza kutoa mwongozo katika kuelekeza raslimali mpya zitawanywe vipi katika wilaya.

## Kutoka katika uwanja wa huduma ya afya: Kulenga malaria

Ugonjwa wa malaria umekuwa ni moja ya magonjwa ambayo yanasababisha vifo vingi vya watu hapa Tanzania, ingawa tiba yake na kinga bado havijapata umuhimu unaostahili katika mipango ya afya ya wilaya. Kabla ya mwaka 1977, hali hii ndivyo ilivyokuwa katika wilaya za Rufiji na Morogoro Vijijini. Leo, shukrani kwa mfumo mpya wa mipango, ugonjwa wa malaria sasa unapewa umuhimu mkubwa. Jedwali linaloonyesha athari ya magonjwa katika wilaya za Rufiji na Morogoro Vijijini kwa mwaka 2000 zinaonyesha kwamba malaria sasa inachukua asili 30 na 31 katika wilaya hizo kwenye kiwango cha magonjwa yanayojitokeza kwa wingi katika kila wilaya. Kiwango kikubwa cha ugonjwa huu kinawakumba zaidi watoto chini ya miaka mitano.

Kwa kujumuisha taarifa hii na kwa kutumia chombo hiki, Timu ya Menejimenti ya Afya katika Halmashauri ya wilaya imetenga fedha kwa kiwango ambacho ni mara tano zaidi kwa kugharamia kinga na tiba ya malaria. Kwa upande wa watoto chini ya miaka mitano, bajeti imeongezwa katika kiwango ambacho ni mara 20.

## Mahali pa kupata habari zaidi

**Kwenye mtandao wa Internet, tafuta TEHIP**
**Web site: www.idrc.ca/tehip**
**Eneo hilo ni sehemu ya District Health Accounts**

**Wasiliana na:**
**Mradi wa Uimarishaji wa Huduma Muhimu za Afya (MUHUMA),**
**Sanduku la Posta 78487,**
**Dar es Salaam, Tanzania**
**Simu: (255) (022) 213 0627, Fax: (255) (022) 211 2068**
**Barua Pepe: admi@tehip.or.tz**